HABARI LEO UK 3.

# Wafugaji wataka sheria za mifugo zirekebishwe

Na Francisca Emmanuel

CHAMA cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kimependekeza sheria zote zinazotumika kukamata, kutaifisha na kupiga minada mifugo inayoingia kwenye hifadhi zirekebishwe ili kuzingatia haki ya kikatiba ya kumiliki mali na afya ya mifugo.

Wamesema ili kukabili tatizo hilo, serikali inapaswa kuweka maeneo maalumu kwa ajili ya malisho ya mifugo ili kuhakikisha usalama wa wafugaji na mifugo yao.

Wakili wa chama hicho, Denis Moses amesema hayo Dar es Salaam jana wakati walipowasilisha mapendekezo yao mbele ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini.

Moses alisema wamependekeza kuwepo kwa maeneo ya wafugaji ambayo yatakuwa na maji na malisho ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Alisema hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji ndio maana kumekuwa na migogoro katika maeneo mbalimbali kama vile Morogoro, wilaya ya Namtumbo na Katavi.

Moses alisema kutokuwepo kwa maeneo hayo kunachangia anguko la kiuchumi kwa wafugaji kwani mifugo hufa na kusababisha umasikini.

Alisema mifugo inapotoka eneo moja kwenda lingine au kuvuka mipaka na kuingia kwenye hifadhi za taifa, wamekuwa wakikamatwa na kutaifishwa bila kujali afya za mifugo na haki ya kikatiba ya kumiliki mali.

"Sio sawa kuingiza mifugo katika hifadhi, na kuna taratibu zilizowekwa na sheria za kulipa Sh 100,000 kama faini tunapendekeza hili suala la kutaifisha mifugo liondolewe," alisema Moses.

Pia wamependekeza kuchukuliwa hatua maofisa wa serikali wanaotuhumiwa kuvunja sheria na kuwanyanyasa wafugaji.

Moses alisema sheria ya msaada na huduma ya polisi sura ya 322 ya mwaka 2002 kifungu namba 47 (7) kinaelezea kuhusu mali isiyo na mmiliki na kwamba wanyama wamekuwa wakitumika kama kifaa cha kufanyia uhalifu.

Alisema sheria hiyo imeweka utaratibu ambao unaelekeza mali yoyote isiyo na mmiliki itangazwe kwenye gazeti au kutolewa notisi ili mwenye mali hiyo ajitokeze jambo ambalo halifuatwi.

"Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20, kifungu namba 35 kinaeleza kwamba mifugo inaweza kutumika kama kifaa cha kutenda makosa," alisema Moses.

Vilevile alisema sheria ya misitu namba 14, 2012 ina onesha kuwa kuna zaidi ya misitu 500 ambayo inapanuliwa kila mara hivyo kuhatarisha maeneo ya wafugaji na sheria ya hifadhi za taifa sura ya 282 kifungu cha 25(1) (d) huruhusu mahakama kutaifisha mali isiyokuwa na mwenyewe.

Pamoja na mambo mengine, wameshauri Sheria ya serikali za mitaa kifungu cha 177 (3) kinatoa mamlaka kwa mkuu wa wilaya kukamata na kuweka mtu mahabusu kiondolewe.

Pia alipendekeza Sheria ya uhujumu uchumi sura ya 200 kifungu cha 36 (2) na (3) na kifungu cha 148 (5) zinazozungumzia kuweka ndani na kuwanyima dhamana watuhumiwa kuondolewa badala yake mshtaka yote yawe na dhamana.

Mkoa wa Arusha, ...

* HABARI LEO UK 8. *

# Polisi yaeleza kiini wizi wa mifugo kukithiri

**Na John Gagarini, Kibaha**

WAMILIKI wa mifugo mkoani Pwani wametakiwa kutomaliza kesi za wizi wa mifugo nje ya mfumo wa sheria, kwani kufanya hivyo hakutamaliza tatizo.

Ushauri huo ulitolewa na Kamishna Msaidizi na Ofisa Polisi Jamii Mkoa wa Pwani, Michael Manumbu alipozungumza baada ya kikao na Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani na wadau, kilichofanyika mjini Kibaha.

Ilibainika kuwa baadhi ya wafugaji wanaokumbana na kadhia ya kuibiwa mifugo, wamekuwa na utaratibu wa kumaliza masuala hayo nje ya mfumo wa kisheria hali inayochochea vitendo vya wizi wa mifugo.

Manumbu alisema kuwa utaratibu huo umekuwa na athari kwani wahusika wa vitendo hivyo vya wizi wamekuwa wakiendeleza vitendo hivyo kwani wanajua hakuna adhabu anayopata.

Alisema wezi wa mifugo wanapobainishwa wafikishwe kwenye vyombo vya sheria ili hatua zichukuliwe bila kujali aliyetenda kosa hilo ni ndugu au rafiki, lazima sheria ichukue mkondo wake ndiyo itamaliza matukio hayo.

"Chanzo kingine cha kuendelea kwa wizi wa mifugo ni wamiliki kutokuwa na kumbukumbu za watu wanaowaajiri kwa ajili ya kuchunga mifugo yao hivyo wachungaji hao kufanya wizi na kushindwa kutambuliwa," alisema Manumbu.

Alisema jambo lingine ni kutokuwa na elimu, ufugaji holela wa makundi makubwa ya ng'ombe na watu wanaowakabidhi kutowafuatilia au kuwasimamia.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, Ngobere Msamau alisema miongoni mwa mikakati waliyoweka ni kutoa tuzo kwa kata inayofanya vizuri kukabiliana na wizi wa mifugo. Pia wametoa hati chafu kwa kata isiyofanya vizuri kwenye mipango ya kuzuia wizi wa mifugo.



Mene... habar... maofi...

Tr...

Na S... Mwa...

H... imep... kipir... uong... ya Si... kiwa... hilo. N... hiyo, taari... hafal... Shul... chan... wan... wa k... A...

kuhakikisha maji yanapatikana muda wote.

# 'Kuanzishwe karakana ya taifa kuchakata ngozi'

**Na Abela Msikula, Mwanza**

WAHADHIRI katika Taasisi ya ufundi Stadi nchini Ethiopia (TVET) wameishauri Tanzania kuanzisha karakana ya taifa ya kuchakata ngozi, ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo.

Wahadhiri hao kwa sasa wako katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Kampasi ya Mwanza, kwa utekelezaji wa programu za kubadilishana ujuzi kati ya taasisi hizo mbili.

Mhadhiri Msaidizi, Selamu Haile, aliliambia gazeti hili jana kwamba karakana ni moja ya soko kuu la ngozi kwa wafugaji.

"Nchini kwetu tunayo. Pamoja na mambo mengine, inasaidia kuzuia upotevu wa ngozi na hivyo kukuza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali," alisema.

Alizitaka mamlaka husika nchini zitoe elimu kwa umma wakati wote, kwa wafugaji kutambua utunzaji wa ngozi mara tu baada ya kuchinja mnyama, ili zifike katika karakana zikiwa katika ubora unaotakiwa.

Alisema elimu hiyo ni pamoja na kuhakikisha ngozi haiwekwi chini/ardhini mara baada ya kuchunwa kwenye mnyama, badala yake ining'inizwe ukutani.

"Inampasa mchuna ngozi kuipaka chumvi ya kutosha ngozi hiyo, endapo hana uhakika wa kuifikisha kwenye karakana ndani ya saa mbili," alisema Haile ambaye yuko DIT kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kutengeneza viatu vya ngozi aina mbalimbali.

kero hiyo ya maji,"alisema Usinga.

yeye na timu ya maafisa wengine wa sekretarieti hiyo ya Azimio la Nairobi

yanalingana na ya nchi nyingine ndipo mradi huu ukaanzishwa na tukaona hatuwezi kuanzisha mradi

matumizi ya binadamu, maji kwa ajili ya Mazingira na maji kwa ajili ya shughuli zingine.

* UHURU UK 16. *

# PAC yaridhishwa uwekezaji kiwanda cha machinjio Mvomero

Morogoro
**NA WARIOBA IGOMBE**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imesema imeridhishwa na hatua za uwekezaji wa kiwanda cha machinjio ya kisasa wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, ambacho kitauza nyama katika soko la nje kwa asilimia 80 na la ndani asilimia 20 kikiwa na matarajio ya kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku.

Hayo yalibainishwa juzi na Makamu Mwenyekiti wa wakati kamati hiyo, ilipokuwa ikikagua kiwanda hicho na kueleza kuwa mbali na kutoa ajira, pia kiwanda kitasaidia kufungua soko la nje na kukabiliana na changamoto za kuwa na mifugo mingi isiyo na tija katika uchumi wa wafugaji na taifa.

"Tuna tatizo la takwimu na pia la mifugo yetu kuuza katika soko la nje, haiwezekani tuwe na idadi kubwa ya mifugo lakini hatuna soko la nje, hiki kiwanda cha machinjio kitaenda kuwa suluhu na leo tumekuja, tumeona, pia tumejifunza kupitia kiwanda hiki,"alisema Hasunga.

Alisema machinjio ya NGURU HILLS ni kiwanda cha kisasa na kwamba kitasaidia kufungua soko la nje na kukabiliana na changamoto za kuwa na mifugo mingi isiyo na tija katika uchumi wa wafugaji wenyewe na taifa zima.

Hasunga alisema kiwanda hicho kitafungua fursa kwa wafugaji kufuga kisasa pia kujiimalisha kiuchumi, ambapo aliwataka wafugaji nchini husus an wa mkoa wa Morogoro kufuga mifugo yenye tija kwa taifa kwenda sambamba na mahitaji ya soko la dunia katika mahitaji ya nyama.

"Soko la nyama duniani linahitaji mifugo bora hivyo ili kuwenda sambamba na ushindani wa soko hilo wafugaji wanatakiwa kufuga mifugo yenye tija na kuepuka kuwa na mrundikano wa mifugo isiyokuwa na tija yoyote,"alisema Hasunga

Mjumbe wa kamati hiyo, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema machinjio hayo yameleta mabadiliko makubwa ya kifikra katika kuchagiza maendeleo sekta ya mifugo kutokana na uwepo wa kiwanda hicho cha kisasa kinachozalisha nyama bora kwa watumiaji na kwa bei rafiki.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF), CPA Hosea Kashimba, alisema kuwa uzalishaji wa nyama kiwandani hapo ulianza tangu mwaka jana na kuzinduliwa rasmi mwezi Desemba 2022.

Kasimba alisema hadi sasa, tayari zaidi ya tani 150 za nyama zimezalishwa zikiwa na thamani zaidi ya bilioni 1.59/- na kwamba kupitia kiwanda hicho cha nyama kimetoa fursa nyingi za ajira kwa wananchi wazawa hususan vijana.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Dk. Aggrey Mlimuka, aliwataka wafugaji kuacha tabia ya kufuga kwa mazoea na badala yake aliwataka wafuge kisasa kuongeza thamani ya mifugo yao katika soko la dunia.

Kiwanda cha kisasa cha Nguru Hills kinanunua ng'ombe kutoka kwa wafugaji kwa kuzingatia umri wa ng'ombe na uzito wake ambapo ng'ombe hukaa kwa miezi mitatu akilishwa vyakula bora ambavyo humfanya anenepe kwa kilo 1.3 kila siku na kuifanya nyama yake kuwa bora na laini katika soko.

CamScanner

Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wa Jiji la Dodoma, wakiandamana kwa ajili ya kupongeza mafanikio ya miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan jijini humo jana.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

fanyabiashara wasipandishe bei ya vyakula katika mwezi huu kama alivyofanya Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

NIPASHE UK 3.

# * Wafugaji watoa mapendekezo 9 Tume ya Hakijinai *

**Na Restuta James**

WAFUGAJI wamewasilisha mapendekezo tisa kwenye Tume ya Rais ya Kurekebisha Mfumo wa Hakijinai, wakitaka serikali itenge maeneo ya malisho na iache kutaifisha mifugo inayoingia kwenye Hifadhi za Taifa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Mrida Mshota, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya kuwasilisha maoni yao mbele ya tume hiyo inayoongozwa na Jaji mstaafu, Othman Chande.

Alisema kutengwa kwa maeneo ya malisho kutaepusha migogoro kati ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi.

Alisema pendekezo hilo linalenga kuwapa wafugaji maeneo yanayokidhi mahitaji yao, kama inavyofanyika kwa wakulima, mapori ya akiba na tengefu; Hifadhi za Taifa na Misitu, akilalamikia kwamba wafugaji wamekuwa wakihamishwa kutoka eneo moja kwenda lingine bila kujali kama lina mahitaji muhimu ambayo ni malisho au maji.

Kadhalika, wametaka maboresho ya sheria tisa wakitaka wakuu wa wilaya wanyang'anywe mamlaka ya kukamata na kuweka watu ndani.

Katika hilo, wametaka Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kifungu cha 177 (3) kifutwe. Kadhalika, wamependekeza Sheria ya Uhujumu Uchumi sura namba 200 kifungu cha 36 (2) na (3) kirekebishwe ili makosa yote yawe na dhamana na Mwendesha Mashtaka (DPP), asiruhusiwe kuzuia dhamana kwa mtuhumiwa yeyote.

Wafugaji wamependekeza pia marekebisho ya Sheria ya Wanyamapori sura ya 283 vifungu vya 18 (4) na 21 (2), kuhusu kukamatwa kwa mifugo inayoingia hifadhini na kwenye mapori tengefu, mapori ya akiba na faini zinazotozwa wakieleza kuwa adhabu ni kubwa.

Alisema sheria hiyo inataka mmiliki wa mifugo aadhibiwe inapoingia kwenye hifadhi na badala yake, inatumika kutoza faini kwa kila ng'ombe, mbuzi au kondoo, anayekutwa kwenye maeneo hayo.

Mwanasheria wa CCWT, Denis Shangai, alitaja sheria nyingine kuwa ni Sheria ya Jeshi la Polisi sura 322 kifungu cha 47 kinachotaka liwekwe tangazo gazetini kwa miezi sita ili mwenye mali hiyo ajitokeze, lakini kinatumiwa vibaya na vyombo vya dola kutaifisha mifugo inayoingia kwenye hifadhi.

Alisema Ibara ya 24 ya Katiba ya mwaka 1977 inazungumzia haki ya kumiliki mali kama moja ya haki za binadamu na kwamba haki hiyo inanyang'anywa na vyombo vya dola vinavyotaifisha mifugo.

"Ukamataji, utaifishaji na uuzaji wa mifugo ni kinyume cha Ibara hii ya Katiba," alisema.

Shangai alitaja sheria nyingine inayowaumiza wafugaji ni ya Hifadhi za Taifa sura ya 282 kifungu 25 (1)(d) na kanuni zake ambazo alidai kinatumiwa vibaya kutaifisha mifugo. Kwa mujibu wa Shangai, sheria nyingine wanayopendekeza irekebishwe ni ya msaada na huduma ya Polisi sura ya 322 (47) (7) na Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2012.